



Uhakiki wa uzito wa bidhaa kwenye kiwanda cha majani ya chai.



Uhakiki wa vipimo kwenye nondo



Vipimo sahihi na vya kuaminika kwa wote.



Uhakiki wa uzito wa mifuko ya saruji (cement)



Uhakiki wa ujazo kwenye bidhaa za vimiminika



Vipimo sahihi na vya kuaminika kwa wote.

Kwa Mawasiliano zaidi;
Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Vipimo,
Vipimo House, S.L.P 2014, Medeli,
Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 262 610 700
Namba ya Bure: 0800 110097
Barua pepe: info@wma.go.tz
Tovuti: www.wma.go.tz
Instagram: [wakalawavipimotanzania](https://www.instagram.com/wakalawavipimotanzania)

**Umuhimu wa kuhakiki
bidhaa zilizofungashwa**



Mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi juu ya Kasha la bidhaa iliyofungashwa (Labelling)

- ✔ Jina (Utambulisho) la bidhaa
- ✔ Jina na mahali unapofanyika ufungashaji
- ✔ Anuani ya posta, Simu, Barua pepe na Nukushi
- ✔ Kiasi halisi cha bidhaa kilichofungashwa bila kujumlisha kifungashio (net content)
- ✔ Uandishi wa ufupisho wa Vipimo (Units), mfano. kg, g, L, l, mL n.k
- ✔ Acha nafasi moja kutenganisha namba na tarakimu mfano: 500 g

MUHMU

Hairuhusiwi katika mazingira ya kawaida, wingi wa bidhaa iliyondani ya Kasha kutumia chini ya asilimia sitini (60%) ya nafasi ya Kasha ili kuepuka uwezekano wa urahisi wa kasha kuweza kumlaghai Mteja kuhusu wingi wa bidhaa iliyomo ndani ya kasha.

Umuhimu wa kuhakiki bidhaa zilizofungashwa

Bidhaa zilizofungashwa ni bidhaa ambazo zimefungashwa na kuandikwa kisia kilichomo na Mzalishaji/Mfungashaji pasipo kushuhudiwa upimaji wake na mnunuzi au mtumiaji wa bidhaa hiyo.

Umuhimu wa kuhakiki bidhaa zilizofungashwa ni:

- Kuwezesha kulindwa kwa Mlaji (Mnunuzi/Mtumiaji) wa bidhaa kwa kupata thamani tarajiwa ya fedha zao kupitia uhakika (assurance) wa usahihi wa kiasi kilichofungashwa na kuandikwa;
- Kuwezesha Wazalishaji/Wafungashaji wa bidhaa wa ndani kufanya biashara kwa uhakika kupitia usahihi wa kiasi kilichofungashwa kuendana na tamko lililoandikwa;
- Kuweshwa bidhaa zilizozalishwa ndani ya nchi kuwa na vigezo vya kiviipimo vinavyokubalika kuingia kwenye ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi ;
- Kuwezesha ushindani wa soko ulio sawa kupitia vigezo vya kiviipimo;
- Kuwezesha Serikali kutoza kodi sahihi kulingana na kiasi sahihi;
- Kuwezesha kuwa na uhakika wa usahihi wa takwimu/makisio yanahusisha kiasi cha bidhaa kilichofungashwa na kuandikwa;



Uhakiki wa bidhaa kwenye kiwanda cha kuuza minofu ya Samaki

Uandishi wa alama sahihi za vipimo katika bidhaa

Uhakika wa muelekeo wa usahihi wa kiasi kilichofungashwa ndani ya kasha huanza na muenekano wa ujazo wa kasha na kufuatiwa na namna ya uandishi wa alama za vipimo juu ya Kasha. Hivyo namna ya uandishi wa alama za vipimo huongeza thamani katika mauzo ya bidhaa. Uandishi wa alama za vipimo unatakiwa kuandikwa kwa usahihi kama jedwali linavyoonesha;-

Jina la alama	Alama sahihi	Alama isiyo sahihi
milimetre	mm	Mm, Mms MM, mms
centimetre	cm	c, Cm, CM, cms
metre	m	M, mt,
kilometre	km	Km, KM, kms, k,K
gram	g	GRM, gm, grm., grms, gr, Grams, GM, GR
kilogram	kg	Kilo, KGM, kgm, kgs, kgms, KGS, KGMS, Kg., KG
Square metre	m ²	Sq. metre, ., M ²
Square millimetre	mm ²	Mm ² , sq.mm
millilitre	ml or mL	ML, MI, mls, MLs,
litre	L or l	, ltr, lts, LTS,
cubic centimetre	cm ³	CM3 ., cc
cubic metre	m ³	M ³ , cu.metre